

Maswali

1. Mbona Wakristo wengi waliuza mashamba na nyumba zao?
2. Mbona Anania na Safira walitaka kupeana pesa kusaidia maskini?
3. Anania na Safira walifanya mpango gani?
4. Anania alipelekea Petro sehemu ya pesa. Alisema uongo gani?
5. Mbona Petro alikasirika?
6. Mungu alikasirika kwa sababu Anania alileta sehemu ya pesa?
7. Nini ilifanyika kwa Anania?
8. Safira aliambia Petro nini?
9. Nini ilifanyika kwa Safira?
10. Tunajifunza nini kwa hii hadithi?

Majibu

1. Walisaidia maskini pesa zao walizouza mashamba zao.
2. Walitaka Wakristo wengine wafikiri kwamba wao ni wazuri.
3. Walipanga kuweka sehemu zingine za pesa na kujifanya wameleta **zote**.
4. Anania aliambia Petro kwamba walikuwa wamepeana pesa **zote** kwa maskini.
5. Petro alikasirika kwa sababu Anania alidanganya Mungu.
6. Hapana. Mungu angefurahi tu kwa sababu walikuwa wamesaidia maskini pesa. Hawakutakiwa walete zote. Mungu alikasirika kwa sababu walikuwa wamedanganya.
7. Anania alianguka chini na akafa. Vijana walimzika.
8. Safira aliambia Petro kwamba walikuwa wamepea maskini pesa zote.
9. Safira alianguka chini na akafa. Vijana walimzika karibu na mmewe.
10. Lazima tuwe waaminifu. Lazima tusaidie wenzetu kwa sababu tunapenda Mungu. Tusingaidie kwa kujionyesha kwa wenzetu ili wafikirie sisi ni wazuri.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 2 Mwaka wa 2

90 Anania na Safira

Kwa Biblia

Matendo ya Mitume mlango wa 5:1 – 11

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anaona kila kitu tunachofanya. Anajua chenye tunafikiria. Anajua sababu gani tunafanya kila kitu. Mungu anataka tusaidie wengine kuonyesha tunampenda.

Somo

Wakristo wengi Yerusalem walitaka kusaidia wasiojiweza. Wakristo wengi waliuza mashamba na nyumba zao. Walisaidia maskini na hizo pesa.

Kulikuwa na Mkristo mmoja aliyeitwa Anania. Mkewe aliitwa Safira. Anania na Safira walitaka watu wengine wafikiri kwamba wao ni wazuri. Waliambia Wakristo wenzao juu ya mambo mazuri waliyoyafanya. Anania na Safira walisaidia watu wengine ikiwa kulikuwa na watu wa kuwaona. Yesu alisema tusingionyeshe tufanye watu wafikirie kwamba sisi ni wazuri. Tufanye mazuri kuonyesha kwamba tunampenda Mungu.

Anania na Safira waliona watu wakiuza mashamba na nyumba zao. Waliona Wakristo wakisaidia maskini kwa kuwapea pesa.

Anania na Safira walifikiri watu watawaona ni wazuri sana wakiuza shamba lao na wasaidie maskini. Anania na Safira walitaka watu wafikirie kwamba wao ni wazuri. Lakini hawakutaka kupeana pesa zao zote. Anania na Safira walikuwa na mpango.

Anania na Safira waliuza shamba na nyumba yao. Walipata pesa nyingi sana. Anania na Safira walipanga kuweka pesa zingine na wapeani kidogo iwasaide maskini. Waliamua kijiwekea pesa zingine. Lakini walisema uongo. Walisema kwamba walikuwa wanapeana pesa **zote** kusaidia maskini. Anania alipea Petro sehemu ya hizo pesa.



Aliambia Petro, "Tumeuza shamba na nyumba yetu. Tumeleta pesa **zote** kusaidia maskini. Tumeleta pesa **zote** tulizo kuwa nazo." Anania alifikiri Petro atafurahi sana. Alifikiri Petro atafikiri kwamba hao ni watu wazuri.

Anania alisahahu kwamba Mungu anajua kila kitu chenye tunafanya. Mungu anajua kila kitu chenye tunafikiria. Mungu alijua kwamba Anania alikuwa anasema uongo. Mungu alijua mpango uliofanywa na Anania na Safira. Mungu alionyesha Petro mpango wenye Anania alikuwa amefanya.

Petro hakufurahi. Alikasirika sana. Aliambia Anania, "Mbona umedanganya Mungu. Shamba lilikuwa lako. Uliamua kuiuza. Uliamua kupeana sehemu ya hizo pesa. Mungu angefurahi kama ungepeana sehemu yake kusaidia maskini. Hakukuwa na makosa kijiwekea sehemu ingine. Lakini ultaka watu wakuone kwamba wewe ni mzuri. Umesema uongo juu ya hizo pesa. Haujasema uongo kwa watu. Umesema uongo kwa Mungu. Mungu ameona vibaya kwa sababu umemdanganya."

Papo hapo Anania alianguka chini na akafa. Vijana walikuja na kumtengeneza. Walimtoa nje na kumzika.

Baada ya masaa matatu, Safira alikuja kwa Petro. Hakuja kilichokuwa kimetendeka kwa Anania. Petro alimuuliza, "Hii ndiyo pesa wewe na Anania mlipata kwa kuza shamba?" " Ndiyo." Safira alijibu. "Tulileta pesa **zote** tulizouza ili tupee maskini."

Petro aliambia Safira, " Mbona mlipanga nyote pamoja kudanganya Mungu? Angalia! Vijana walioenda kuzika Anania wamerudi. Watakuza hata wewe."

Safira alianguka chini na akafa. Vijana walimzika karibu na mmewe.



Mungu anataka tumpende. Anataka tuonyeshe huo upenda kwa kupenda watu wenzetu. Mungu hufurahi tukisaidia wenzetu walio na shida. Mungu anataka tusaidie wenzetu kwa sababu tunampenda.

Wakati wote Mungu anajua tunachowaza, tunachosema na tunachofanya. Hatuwezi kudanganya Mungu. Mungu hafurahii tukisaidia wenzetu tukitaka watu wajue kwamba sisi ni wazuri. Mungu anataka tusaidie wenzetu tuonyeshe kwamba tunampenda.

Mungu anajua tukidanganya. Tunaweza kudanganya wengine lakini hatuwezi kudanganya Mungu. Tujaribu sana tupende Mungu. Tuonyeshe kwamba tunapenda Mungu kwa kusaidia wenzetu.